


OFISI YA KUTATUA MIZOZO

Mkutano wa Maafikiano wa Maafisa wa Usikilizaji



Mwongozo wa Wazazi

Mkutano wa Maafikiano wa Maafisa wa Usikilizaji (HOSC) Ni Nini?

Mkutano wa Maafikiano wa Maafisa wa Usikilizaji (HOSC) ni huduma ambayo wahusika ambao wako karibu kupata suluhisho, lakini wametambua vikwazo/vizuizi, wanaweza kushirikiana na Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano ili kuona ikiwa vikwazo/vizuizi hivyo vinaweza kutatuliwa ili wahusika waweze kuepuka usikilizaji na kupata suluhisho.

Huduma za Ofisi ya Kutatua Mizozo

Wazazi na shule zina njia kadhaa za kutatua kutoelewana kwao kuhusu elimu maalum ya mtoto:

- Huenda mzazi au shule ikaomba Uwezeshaji wa Mpango Uliobinafsishwa wa Elimu (IEP).
- Huenda mzazi au shule ikaomba Upatanishi.
- Huenda mzazi au shule ikaomba Usikilizaji wa Kisheria.

Wakati mzazi au shule imeomba Usikilizaji wa Kisheria, Ofisi ya Kutatua Mizozo (ODR) hupeana maafisa wawili wa usikilizaji kwa kesi hiyo:

- **Afisa wa Usikilizaji wa Kisheria:** Afisa wa Usikilizaji wa Kisheria hupanga usikilizaji wa kisheria; husikiliza mashahidi na huangalia hati; na huandika uamuzi, na kuamua jinsi kutoelewana huko kunapaswa kuzinduliwa.
- **Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano:** Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano hupanga HOSC na uhusika tu ikiwa mzazi na shule wataomba HOSC. Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano husaidia mzazi na shule kujaribu kutatua kutoelewana kwao, ili wasipitie usikilizaji. Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano anaweza pia kuitwa Afisa wa Usikilizaji wa HOSC.

Kushiriki katika HOSC hakughairi usikilizaji wa kisheria. Usikilizaji wa kisheria husalia umepangwa isipokuwa wahusika wamweleze Afisa wa Usikilizaji wa Kisheria kwamba kesi hiyo imetatuliwa na usikilizaji hauhitajiki.

Hapa kuna baadhi ya mambo muhimu ya kukumbuka:

- Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano ni mmoja wa maafisa wa usikilizaji kutoka ODR (<http://odr-pa.org/due-process/hearing-officers>) kwa hivyo ana ufahamu na tajriba ya kutoelewana ya elimu maalum.
- HOSC inaweza kumpa mzazi na shule mitazamo kuhusu matatizo na vikwazo ambavyo vinazuia maafikiano.
- Mchakato wa HOSC hufanyika kupitia simu, kwa hivyo ni rahisi kupanga na ni wa faragha kabisa. Afisa wa Usikilizaji wa Kisheria hataambiwa kuhusu majadiliano na mzazi au shule wakati wa HOSC.
- Mchakato wa HOSC hufanyika tu ikiwa wazazi wote na shule wanataka kushiriki. Hakuna mhusika yeyote atalazimishwa kushiriki katika HOSC.

Washiriki wa HOSC ni pamoja na Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano na yeyote kati ya wafuatao:

- Wazazi au Walezi wa mtoto
- Wakili wa mzazi (ikiwa ana mmoja; **Wazazi hawahitaji wakili ili kuwa HOSC**)
- Wawakilishi wa shule
- Wakili wa shule

Kulingana na hali ya kutoelewana, Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano ataamua ni nani atashiriki katika HOSC.

Kuandaa Mkutano wa Maafikiano wa Maafisa wa Usikilizaji

Ni vyema kwa kila mtu wakati wazazi na shule wanaweza **kushirikiana kwa pamoja** kufanya maamuzi ya kielimu kuhusu mtoto **kwa pamoja**. Mzazi anamjua mtoto vizuri, na shule wana utaalamu na ufahamu kuhusu kuwafunza watoto wenye ulemavu. **Kwa pamoja**, ni timu yenye nguvu.

HOSC ya kawaida itafanyika hivi:

- 1) Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano atapanga simu ya mkutano na kila mtu. Wakati wa simu ya kwanza, Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano ataongea na wahusika wote ili kujua jinsi anavyoweza kusaidia vizuri wazazi na shule katika kuongea kuhusu kutoelewana kwao, na ikiwezekana kuafikia makubaliano.
- 2) Baada ya siku ya kwanza, Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano atapanga simu za faragha na wazazi, na, tofauti, na shule. Hii inamaanisha Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano hataambia shule ni nini wazazi walisema, au kuwaeleza wazazi yale shule ilisema.
- 3) Simu za ziada zitapigwa kama itakavyohitajika. Lengo la mchakato litakuwa kwa Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano kuwasaidia wazazi na shule kutambua kama kuna njia ya kutatua kutoelewana bila hitaji la usikilizaji wa kisheria.

Vidokezo vya Kuandaa HOSC (kwa wazazi ambao hawana wakili)

- Elewa hoja katika kesi yako. Je, kutokukubaliana huku kunahusu nini?
- Fikiria kuhusu uwezo na udhaifu wa kesi yako.
 - Madai yako ni gani?
 - Madai ya shule ni gani?
- Fikiria kuhusu jinsi unavyoweza kufafanua vyema kesi hiyo kwa Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano.
 - Kwa nini hujaridhishwa na mpango wa sasa wa elimu wa mtoto wako?
 - Ugependa kuona nini kikifanyika na mpango wa elimu wa mtoto wako ambacho hakifanyiki sasa?
 - Ni kwa nini unaamini sheria inaunga mkono msimamo wako?
- Jiandie kutoa muhtasari mfupi wa kusimulia wa kesi hiyo kwa Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano. Huenda ukataka kuandika muhtasari huu, na utumie manukuu wakati unaongea na Afisa wa Usikilizaji wa Maafikiano.

Rasilimali

Kuna rasilimali nyingi za wazazi zilizo rodheshwa katika *Ilani ya Kulinda Utaratibu*. Unaweza kupata *Ilani ya Kulinda Utaratibu* kwenye tovuti ya PaTTAN website: www.pattan.net

Wataalamu wa ConsultLine wanaweza kuongea na wewe kuhusu sheria na masharti ya elimu maalum ambayo yanatumika kwa kesi yako: 800-879-2301. Watumiaji wa TTY: PA Relay 711 au <http://odr-pa.org/parents/consultline/>

- Maktaba ya Rasilimali za Wazazi ya ODR y anajumuisha sheria na sera za jimbo na serikali: <http://odr-pa.org/parents/parent-resource-library/>
- *Usikilizaji wa Kisheria wa Elimu Maalum, Mwongozo wa Wazazi* una maelezo muhimu kuhusu mada mbalimbali. http://odr-pa.org/wp-content/uploads/pdf/DPH_parent_guide.pdf
- Maamuzi ya afisa wa usikilizaji yanapatikana mtandaoni na yanaweza kutafutwa kulingana na matatizo: <http://odr-pa.org/due-process/hearing-officer-decisions/>



OFFICE FOR DISPUTE RESOLUTION
6340 Flank Drive
Harrisburg, PA 17112-2764

(800) 222-3353 (717) 901-2145
WATUMIAJI WA TTY: PA Relay 711

www.odr-pa.org



pennsylvania
DEPARTMENT OF EDUCATION

Kupitia Ofisi ya Kutatua Mizozo, Idara ya Pennsylvania ya Elimu (PDD) inatimiza wajibu wa kisheria wa kudumisha mfumo wa mchakato wa kusikiliza wa elimu maalum. PDE hushirikiana na Central Susquehanna Intermediate Unit kutoa msaada wa hazina ya serikali na wa usimamizi wa ofisi hiyo, bila kuhusika katika shughuli.

The Central Susquehanna Intermediate Unit haitabagua katika mipango ya elimu, shughuli au ajira kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, jinsia, ulemavu, hali ya ndoa, dini, mapendeleo ya kimapenzi, ukoo, uanachama wa chama cha wafanyakazi, au ainisho nyingine za kisheria zinazolindwa. Tangazo la sera hii linalingana na Title VI ya Sheria ya Haki za Wananchi ya 1964, Title IX ya Marekebisho ya Elimu ya 1972, Sehemu ya 504 ya Sheria ya Urekebishaji Tabia ya 1973, na Sheria ya Wamerikani wenye Ulemavu ya 1990. Wafanyakazi na washiriki wa mpango ambao wana swali au malalamiko ya unyanyasaji au ulemavu, au ambao wanahitaji maelezo kuhusu kuwakimu watu wenye ulemavu, wanapaswa kuwasiliana na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, CSIU, 90 Lawton Lane, Milton, PA 17847, 570-523-1155.